# INTERNATIONAL STAR ASSESSMENT

# KUTATHMINI HATUA ZA MWANAFUNZI

## GREDI YA SITA - MWAKA 2025

## KISWAHILI

**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali 1-5.**

**Kubai:** Shikamoo baba?
**Baba:** Marahaba mwanangu! Habari za shule?
**Kubai:** Njema baba! Baba nikueleze kitu?
**Baba:** Naam, nieleze mwanangu.
**Kubai:** Wenzangu walinichagua kuwa kiranja mkuu wa darasa.
**Baba:** Hongera mwanangu.
**Kubai:** Sijui ninastahili kufanya nini ili niwe kiongozi bora?
**Baba:** Unastahili kuwa na upendo na uonyeshe heshima kwa wote bila kubagua.
**Kubai:** Kweli baba, pia ninastahili kuwa mwaminifu.
**Baba:** Vyema! Nidhamu yako lazima iwe nzuri, ili uwe mfano mwema kwa wenzako.
**Kubai:** Asante baba. Hakika umenifunza mengi.

1. Kubai alipoulizwa na baba kuhusu habari za shule, alimjibu________
   A. shikamoo
   B. naam
   C. njema
   D. marahaba
2. Ni jibu lipi linaonyesha maadili ambayo baba alimfunza Kubai?
   A. Upendo, heshima na nidhamu njema
   B. Mwaminifu, nidhamu bora, hongera
   C. Uaminifu, maamkuzi, tabia
   D. Heshima, marahaba, upendo
3. Maneno yafuatayo yametumika katika mazungumzo. Lipi halionyeshi adabu?
   A. Asante
   B. Kiranja
   C. Naam
   D. shikamoo
4. Kubai anafaa kufanya nini baada ya kuzungumza na baba yake?
   A. Kuwapongeza waliomchagua kuwa kiranja
   B. Kuwaeleza mawaidha aliyopewa na babaye
   C. Atazingatia mawaidha ya baba
   D. Atabadilisha sheria za shule
5. Ni nani aliyemwamkua mwenzake shikamoo?
   A. Kubai
   B. Kiranja
   C. Mwalimu
   D. Baba

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 6 hadi 9.***

Duale alikuwa mtoto wa kiume na kifungua mimba katika familia ya watoto wanne. Yeye alikuwa katika darasa la sita wakati babaye aliposhikwa na ugonjwa mbaya na hatimaye kuaga dunia. Mwaka mmoja baadaye, mama naye akamfuata baba. Sasa jukumu la kuwalea nduguze wadogo likabakia mabegani mwake.

Kuhudhuria kwake shuleni kukaanza kuwa kugumu. Alianza kukosakosa kuhudhuria kwa minajili ya kuwahudumia wenzake.

6. Kifungua mimba ni mtoto yupi?
   A. Aliyezaliwa akiwa wa mwisho
   B. Aliyezaliwa wa pili katika familia
   C. Aliyezaliwa wa kwanza
   D. Mtoto wa katikati
7. Kwa nini jukumu la kuwalea nduguze lilibakia mabegani mwa Duale?
   A. Kwa sababu ya kifo cha baba
   B. Kwa sababu ya kifo cha mama
   C. Kwa sababu alikuwa ameajiriwa kazi
   D. Kwa sababu ya vifo vya wazazi wote
8. Duale alianza kukosakosa shuleni ili.
   A. iliatafute kazi
   B. ili awahudumie wenzake
   C. kazi ya shule ilikuwa nyingi
   D. aliambiwa na walimu awache shule
9. Kuaga dunia inamaanisha
   A. kuwa mgonjwa
   B. kuambia watu kwaheri
   C. kufariki
   D. kuzikwa
10. Ni mzazi yupi aliyeaga dunia kwanza?
   A. Baba
   B. Mama
   C. Babu
   D. Mjomba

***Soma kifungu hiki kisha ujibu swali la 11 hadi 15***

Miwa ni moja kati ya mimea inayotegemewa na watu wengi. Kuna wale wanaoitumia kutengeneza sharubati. Je, unafahamu kuwa, sharubati inayotokana na miwa inaweza kuzuia magonjwa kama vile kansa? Asilimia kubwa ya miwa inayokuzwa ulimwenguni hutumiwa kutengeneza sukari inayotumiwa nyumbani, hotelini na viwandani. Watu wengi hupenda kunywa chai moto iliyotiwa sukari hasa baridi inapozidi. Hata hivyo, wapo wanaopenda asali badala ya sukari. Je, unapenda asali ikitiwa katika chai?

11. Taja mimea inayotumika kutengeza sukari?
   A. Sharubati
   B. Mhogo
   C. Sukari mti
   D. Miwa
12. Ugonjwa upi unaweza tibiwa na sharubati iliyotengenezwa na miwa?
   A. Ugonjwa wa sukari
   B. Kifua kikuu
   C. Kansa
   D. Korona
13. Sukari hutumika katika sehemu zifuatazo isipokuwa
   A. hotelini
   B. usafirini
   C. nyumbani
   D. viwandani
14. Watu wengi hupenda kunywa chai moto iliyotiwa sukari hasa wakati gani?
   A. kila siku
   B. wakati wa joto jingi
   C. Ikiwa na asali
   D. baridi inapozidi
15. Kichwa mwafaka cha kifungu hiki ni
   A. Matumizi ya miwa
   B. Ugonjwa wa kansa
   C. Umuhimu wa sukari
   D. Umuhimu wa asali

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 16 hadi 20. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa***

Uhai _____16_____ binadamu hutegemea sana maji, chakula na hewa. _____17_____ kwa mahitaji makuu haya ndiko _____18_____ mtu _______19 _________ kama ______ 20 ______.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 16. | A. ya | B. cha | C. wa | D. la |
| 17. | A. Kumiliki | B. Kukamilika | C. Kukamilikia | D. Kumulika |
| 18. | A. kunamfanya | B. kunakomfanya | C. kinalomfanya | D. kunaomfanya |
| 19. | A. awe | B. asiwe | C. akule | D. asikue |
| 20. | A. anaonekana | B. anavyoonekana | C.aonekane | D. huonekana |

***Kutoka swali la 21 hadi la 30, chagua jibu sahihi***

21. Kamilisha: Safu ya _________
    A. mti
    B. wanafunzi
    C. siafu
    D. askari

22. Kamilisha methali ifuatayo;
    Mtaka cha mvunguni sharti ________
    A. atafute
    B. apande
    C. hachoki
    D. ainame

23. Tumia nahau inayofaa kujaza pengo
    Tuli ________ _________ darasa letu likawa safi.
    A. futa vumbi
    B. piga pasi
    C. piga deki
    D. piga mswaki

24. Chagua wingi wa sentensi hii.
    Mwalimu ametupatia cheti
    A. Mwalimu ametupatia vyeti
    B. Walimu wametupatia vyeti
    C. Walimu wametupatia cheti
    D. Walimu wametupatia vieti

25. Ukubwa wa neno ngamia
    A. gamia
    B. ngamia
    C. kingamia
    D. jingamia

26. Kamilisha tashbihi ifuatayo
    Msichana yule ni mpole kama _____
    A. malaika
    B. mwanambuzi
    C. mwanakondoo
    D. maji

27. Chagua kinyume cha sentensi hii:
    Wanafunzi walishuka basi
    B. Wanafunzi walipaa basi
    B. Mwanafunzi alishuka basi
    C. Wanafunzi alipanda basi
    D. Wanafunzi walipanda basi

28. Ni kitenzi kipi kiko katika hali ya kutendana?
    A. Rukiwa
    B. Kunjana
    C. Chorewa
    D. Funika

29. Andika sentensi hii kwa umoja;
    Magonjwa yalikabiliwa vilivyo
    A. Gonjwa lilikabiliwa vilivyo.
    B. Magonjwa yalikabiliwa vilivyo.
    C. Ugonjwa ilikabiliwa vilivyo.
    D. Ugonjwa ulikabiliwa vilivyo.

30. Kiungo kipi cha mwili huondoa uchafu kwenye damu?
    A. Mifupa
    B. Figo
    C. Moyo
    D. Ini

Mwandikie rafiki yako barua ukimweleza jinsi likizo ya Disemba ilivyokuwa.